
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

# MWONGOZO WA UPATIKANAJI, UENDELEZAJI NA USIMAMIZI WA MAENEO YA MALISHO



DESEMBA, 2021

# MWONGOZO WA UPATIKANAJI, UENDELEZAJI NA USIMAMIZI WA MAENEO YA MALISHO

**DESEMBA, 2021**

# YALIYOMO


**YALIYOMO** .......... i

**DIBAJI** .......... iv

MUHTASARI .......... vi

SHUKRANI .......... viii

VIFUPISHO VYA MANENO .......... ix

**SURA YA KWANZA** .......... 1

1.0 UTANGULIZI .......... 1

1.1. Lengo la Mwongozo .......... 3

1.2. Chimbuko la Mwongozo .......... 3

**SURA YA PILI** .......... 5

2.0 UPATIKANAJI WA MAENEO YA MALISHO .......... 5

2.1 Utaratibu wa Upatikanaji wa Maeneo ya Malisho katika Vijiji .......... 5

2.1.1 Majukumu muhimu ngazi ya Halmashauri .......... 6

2.1.2 Majukumu muhimu ngazi ya Kijiji .......... 7

2.1.3 Uundwaji wa Kamati ya Usimamizi wa Malisho ya Kijiji .......... 8

2.1.4 Majukumu ya Kamati ya Usimamizi wa Malisho ya kijiji .......... 9

2.1.5 Wajibu na majukumu ya wafugaji katika kutunza na kuendeleza eneo la malisho la kijiji .......... 10

2.2 Utaratibu wa Upatikanaji wa Maeneo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Ngazi ya Halmashauri .......... 15

2.2.1 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri .......... 15

2.2.2 Majukumu ya Kamati ya uhamasishaji wa upatikanaji wa maeneo ya malisho ........ 16
2.2.3 Utaratibu wa upangishaji wa vitalu ........ 16
2.2.4 Majukumu ya mfugaji baada ya kupangishwa kitalu ........ 17
2.2.5 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri kwenye maeneo ya vitalu ........ 21
2.2.6 Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye maeneo ya vitalu ........ 22
2.2.7 Mchanganuo na idadi ya vitalu ........ 22
2.3 Utaratibu wa Upatikanaji wa Maeneo Yaliyoainishwa na Taasisi za Serikali ........ 23
2.3.1 Utaratibu wa upangishaji wa kitalu ........ 24
2.3.2 Majukumu ya mfugaji baada ya kukabidhiwa kitalu ........ 25
2.3.3 Majukumu ya Taasisi kwenye maeneo ya vitalu ........ 27
2.3.4 Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye maeneo ya vitalu kutoka kwenye mashamba ya Taasisi ........ 27
2.3.5 Mchanganuo na Idadi ya Vitalu ........ 28
**SURA YA TATU ........ 29**
3.0 UMILIKI WA MAENEO YA MALISHO ........ 29
3.1 Faida za Umiliki wa Maeneo ya Malisho ........ 31
**SURA YA NNE ........ 32**
4.0 USIMAMIZI NA MATUMIZI ENDELEVU YA MAENEO YA MALISHO ........ 32
4.1 Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho ........ 33
4.2 Usimamizi wa Maeneo ya Malisho ........ 34
4.3 Kamati za Usimamizi wa Maeneo ya Malisho ........ 35

4.3.1 Majukumu ya wadau katika upatikanaji, usimamizi na uendelezaji wa malisho na mbegu za malisho. ................ 37

4.3.2 Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika upatikanaji wa mbegu za malisho. ................................................ 38

4.3.3 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri katika upatikanaji wa mbegu za malisho. ............ 39

4.3.4 Majukumu ya Wafugaji katika upatikanaji wa mbegu za malisho. ................................................ 39

**SURA YA TANO** ................................................ 41

5.0 UPATIKANAJI NA USIMAMIZI WA MAJI KWA MIFUGO .......... 41

5.1 Upatikanaji wa Maji. ................................................ 41

5.2 Majukumu ya Wadau katika Upatikanaji wa Maji kwa Mifugo. .. 42

5.2.1 Majukumu ya Wafugaji ................................................ 42

5.2.2 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri ................................................ 43

5.2.3 Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ......................... 43

5.2.4 Majukumu ya Wizara ya Maji ................................................ 44

5.3 Usimamizi wa Miundombinu ya Maji kwa ajili ya Mifugo .......... 44

5.3.1 Majukumu ya Kamati katika kusimamia na kuhifadhi miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo ......................... 44

**SURA YA SITA** ................................................ 47

6.0 SHERIA ZITAKAZOTUMIKA PAMOJA NA MWONGOZO HUU 47

6.1 Maadili ya Kuzingatia katika Utekelezaji wa Mwongozo ............ 49

**SURA YA SABA** ................................................ 50

7.0 MATOKEO TARAJIWA YA MWONGOZO ......................... 50

# DIBAJI

Malisho ni chanzo kikuu cha chakula cha mifugo wacheuao (ruminants). Nchini Tanzania sehemu kubwa ya malisho inapatikana kwenye maeneo ya malisho ya pamoja (communal grazing land), ambayo kwa muda mrefu yamekuwa hayana uangalizi wala uendelezaji. Maeneo hayo hutoa kiwango kikubwa cha lishe, maji na madini muhimu kwa afya ya mifugo. Hivyo, ni vema wafugaji kuwa na maeneo ya malisho yaliyotengwa na kutambuliwa kisheria kama inavyoelekezwa kwenye Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006, Mkakati wa Upatikanaji wa Uhakika wa Malisho na Maji kwa Mifugo wa mwaka 2018/2019 na Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura Na.180 pamoja na kanuni zake zinazoelekeza uwepo wa usimamizi thabiti wa maeneo ya malisho.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeandaa Mwongozo wa Upatikanaji, Usimamizi na Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho kwa Mifugo ili kutekeleza Sera na Sheria za mifugo pamoja na Maelekezo ya Ilani ya Chama Tawala. Mwongozo huu unaelekeza namna bora ya upatikanaji wa maeneo ya malisho, usimamizi na uendelezaji wa maeneo hayo kwa lengo la kuboresha uzalishaji wenye tija unaoweza kuongeza kipato cha wafugaji na taifa kwa ujumla. Mwongozo pia unasisitiza uwepo wa miundombinu muhimu ya ufugaji ili kupunguza adha ya malisho na maji katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo ili kuwa na uendelevu wa ufugaji na kuondoa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Usimamizi na utekelezaji wa Mwongozo huu utakuwa chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais

TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maji, Wafugaji, Chama cha Wafugaji na wadau wengine. Aidha, Mwongozo huu unamwelekeza kila mdau kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa ili kuchangia na kuboresha mfumo mzima wa ufugaji.

Hivyo, ni matumaini yangu kuwa utekelezaji wa Mwongozo huu utaongeza upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo, ulinzi na usimamizi wa maeneo hayo pamoja na uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho nchini hivyo kuondoa migogoro isiyo ya lazima baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

**Mashimba M. Ndaki (Mb.)**
**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**

# MUHTASARI

Mwongozo huu umeandaliwa kwa lengo la kuelekeza namna ya upatikanaji, umiliki, uendelezaji na usimamizi wa maeneo ya malisho nchini. Vile vile, kuimarisha na kusimamia upatikanaji wa mbegu bora za malisho, kuzuia na kudhibiti kuenea kwa mimea vamizi/magugu sumbufu katika maeneo ya malisho. Mwongozo pia, unaelekeza wajibu na majukumu ya watumiaji na wasimamizi wa maeneo ya malisho wakiwemo Wafugaji, Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Mikoa, Taasisi za Serikali na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mwongozo unaelezea majukumu ya kamati mbalimbali za uhamasishaji wa upatikanaji, usimamizi na uendelezaji wa maeneo ya malisho.

Maeneo ya malisho yanapatikana kupitia Sheria ya Ardhi ya Vijiji Sura Na.114 na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji Sura Na.116. Pia hupatikana kutokana na maeneo ambayo Serikali, Taasisi au wadau wanayatoa kwa ajili ya malisho na maeneo ya mashamba yaliyofutiwa hati ya umiliki wa awali na kutengwa kwa ajili ya malisho na maeneo binafsi yanayomilikiwa na wafugaji na yanatumika kwa shughuli za ufugaji.

Maeneo yaliyopatikana na yatakayoendelea kupatikana yatatengwa, yatapimwa na kuwekwa alama za mipaka za kudumu zinazoonekana. Maeneo hayo yatasajiliwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali na hayatatumika kwa matumizi mengine yasiyokuwa ya malisho kama inavyoelekezwa kwenye Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura Na. 180. Aidha, Mwongozo unaelezea majukumu ya wadau na kamati

mbalimbali katika kuhakikisha upatikanaji na usimamizi wa miundombinu ya maji kwa mifugo. Vile vile, mwongozo umeainisha Sheria na Kanuni mbalimbali zitakazotumika.

Matokeo tarajiwa ya mwongozo huu ni pamoja na uwepo wa uhakika wa malisho na maji kwa mifugo, kupungua kwa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, uwepo wa ufugaji wa kisasa na wenye tija, ongezeko la uzalishaji wa mbegu za malisho, uundaji wa ushirika wa wafugaji, kuwepo kwa utii wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusu upatikanaji, uendelezaji, usimamizi na ulinzi wa maeneo ya malisho.

Rwiguza.

Dkt. Asimwe L. Rwiguza

**MKURUGENZI WA UENDELEZAJI WA MAENEO YA MALISHO NA RASILIMALI ZA VYAKULA VYA WANYAMA**

# SHUKRANI

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inapenda kutoa shukrani za dhati kwa wadau wote walioshiriki kwa kujitolea muda, mali na maarifa yao katika hatua za maandalizi hadi ukamilishwaji wa mwongozo huu. Walioshiriki ni wengi na sio rahisi kuwataja wote kwa majina.

Vile vile, Wizara inatoa shukrani kwa waliohudhuria katika vikao mbalimbali vya maandalizi wakiwemo wataalam wa mifugo, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ambao bila michango yao ya mawazo na uzoefu mwongozo huu usingekamilika.

Shukurani za kipekee ziwaendee Kamati ya wataalaam waliofanikisha uandaaji wa Mwongozo huu, pamoja na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ya *Tanzania Natural Resource Forum* (TNRF), *Ujamaa Community Resource Team* (UCRT), *Tanzania People and Wildlife* (TPW) na KINNAPA kwa kuwezesha uandaaji na uchapishwaji wa mwongozo huu.

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| CCRO | Customary Certificate Right of Occupancy |
| DGLF | Directorate of Grazing Land and Animal Feed Resources |
| DRTE | Directorate of Research, Training and Extension |
| GPS | Global Position System |
| GRO | Granted Right of Occupancy |
| Ha. | Hekta |
| KINNAPA | Muunganiko wa vijiji vya Kiman, Ndaleta, Namelok na Patimbo |
| LU | Livestock Unit |
| NAFORMA | National Forestry Resources Monitoring and Assesment |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PLUM | Participatory Land Use Management |
| TALIRI | Tanzania Livestock Research Institute |
| TNRF | Tanzania Natural Resource Forum |
| TOSCI | Tanzania Official Seed Certification Institute |
| TPW | Tanzania People and Wildlife |
| UCRT | Ujamaa Community Resource Team |
| VLUM | Village Land Use Management |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Tanzania ina jumla ya hekta milioni 94 za rasilimali ya ardhi, kati ya hizo hekta milioni 50 zinaweza kutumika kwa malisho na inakadiriwa kuwa asimilia 35 iko katika maeneo ya nyanda kame chini ya ukanda wa ikolojia iii - iv (zenye mvua kiasi). Kutokana na Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (National Land Use Framework Plan) wa mwaka 2013-2033 unaonesha kuwa eneo la malisho lilikuwa na ukubwa wa hekta 9,829,700 sawa na asilimia 10.3 ya eneo lote nchini. Vile vile, tathmini iliyofanywa na National Forest Resources Monitoring and Assesment (NAFORMA) ya mwaka 2015 inaonesha kwamba eneo linalotumika kwa ajili ya malisho ni takriban hekta milioni 9.3.

Maeneo ya malisho yamekuwa yakipungua na kupoteza ubora wake kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watu na mifugo. Wakati wa uhuru watu walikuwa milioni 9 na mifugo milioni 8, mwaka 2020/2021 inakadiriwa kuwepo watu milioni 60 na mifugo milioni 33.9. Ongezeko hilo la watu na mifugo nchini limesababisha kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi kwa ajili ya makazi, kilimo, ufugaji na shughuli nyingine za kijamii na kiuchumi.

Tanzania inakadiriwa kuwa na kaya milioni 7.7 zinazojihusisha na kilimo, ufugaji na uvuvi ambapo kaya milioni 2.7 sawa na asilimia 35 zinajihusisha na kilimo na ufugaji (NSCA, 2019/2020). Aidha,

kumekuwa na ongezeko la mifugo nchini kufikia takriban ng'ombe milioni 33.9, mbuzi milioni 24.5, kondoo milioni 8.5 na punda takriban milioni 0.7 (Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2021/2022) idadi hii ya mifugo ni sawa na uniti za mifugo (LU) milioni 41.2. Mahitaji ya maeneo ya malisho kwa idadi hiyo ni jumla ya Hekta milioni 103 hii inaonesha upungufu ikilinganishwa na eneo la nchi lililopo. Hivyo, basi inahitajika kujipanga vizuri katika kutumia maeneo yaliyopo ili kuhakikisha uendelevu wa matumizi ya maeneo hayo, tija katika uzalishaji na kuondokana na migogoro isiyo ya lazima.

Changamoto nyingine zinazosababisha kupungua kwa maeneo ya malisho ni pamoja na kubadilisha matumizi ya maeneo ya malisho, kutotekelezwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi, vijiji kukosa mipango ya matumizi ya ardhi, maeneo ya malisho kutoendelezwa na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hivyo, kusababisha wafugaji kuhamahama kutoka kwenye maeneo yao ya asili wakitafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo bila kuacha ulinzi wa maeneo hayo na kusababisha migogoro ya matumizi ya ardhi baina yao na watumiaji wengine wa ardhi.

Kutokana na changamoto hizo, Serikali imeendelea kutekeleza majukumu mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kuna upatikanaji wa uhakika wa maeneo ya malisho, maji na huduma nyingine za mifugo kwa ajili ya ufugaji wenye tija. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali inafanya jitihada za kulinda maeneo hayo kwa kuyaainisha, kuyasajili na kuyatangaza kwenye Gazeti la Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya

Wanyama Sura Na. 180, ili yaweze kutumika kwa utaratibu maalumu utakaowezesha wafugaji kufuga kibiashara na kupunguza vifo vya mifugo wakati wa ukame.

### 1.1. Lengo la Mwongozo

Mwongozo huu unalenga kuelekeza namna ya upatikanaji, umiliki, usimamizi na uendelezaji wa maeneo ya malisho. Vile vile, kuimarisha na kusimamia upatikanaji wa mbegu bora za malisho, kuzuia na kudhibiti kuenea kwa mimea vamizi/magugu sumbufu katika maeneo ya malisho. Pia, unaelekeza wajibu na majukumu ya watumiaji na wasimamizi wakiwemo Wafugaji, Wamiliki wa maeneo ya malisho, Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Mikoa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

### 1.2. Chimbuko la Mwongozo

Mwongozo huu ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006, Mkakati wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wa Upatikanaji wa Uhakika wa Malisho na Maji kwa Mifugo na Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura Na. 180 pamoja na Kanuni zake. Sheria pia inabainisha katika kifungu Na. 06 kuwa miongozo na maelekezo kuhusu usimamizi wa Maeneo ya Malisho yatatolewa ambapo kifungu Na. 16 kinatoa mamlaka ya kusajili maeneo hayo na baada ya usajili kuyatangaza kwenye Gazeti la Serikali ili yaweze kulindwa kwa mujibu wa sheria hiyo. Aidha, kifungu Na. 19 kinaelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa mipango kina ya usimamizi wa maeneo ya malisho yaliyopatikana kupitia Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Sura Na.116.

Pia mwongozo huu umezingatia uzoefu wa miradi mbalimbali ya wadau ya upatakanaji, uendelezaji na usimamizi shirikishi wa maeneo ya malisho.

# SURA YA PILI

## 2.0 UPATIKANAJI WA MAENEO YA MALISHO

Maeneo ya malisho yanapatikana kupitia Sheria ya Ardhi ya Vijiji Sura Na.114 na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji Sura Na.116. Vile vile, maeneo ambayo Serikali, Taasisi au wadau wanayatoa kwa ajili ya malisho na maeneo ya mashamba yaliyofutiwa hati ya umiliki wa awali na kutengwa kwa ajili ya malisho na maeneo binafsi yanayomilikiwa na wafugaji na yanatumika kwa shughuli za ufugaji.

Maeneo yaliyopatikana na yatakayoendelea kupatikana yatatengwa, yatapimwa na kuwekwa alama za mipaka za kudumu zinazoonekana. Maeneo hayo yatasajiliwa, yatatungiwa Kanuni na Taratibu za Usimamizi na hayatatumika kwa matumizi mengine yasiyokuwa ya malisho kama inavyoelekezwa kwenye Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura Na. 180 kifungu Na. 17 (3). Maeneo hayo yatasajiliwa kwa mujibu wa Sheria hiyo na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Maeneo ya malisho yanayolengwa kutangazwa ni yale yaliyoainishwa na vijiji, Halmashauri za Wilaya, Taasisi za umma na mashamba yaliyofutiwa umiliki na kutolewa kwa ajili ya malisho. Aidha, mashamba yaliyopatikana kwa juhudi binafsi za wafugaji (Kununua, kurithi n.k) na yanatumika kwa ajili ya malisho nayo yatasajiliwa.

### 2.1 Utaratibu wa Upatikanaji wa Maeneo ya Malisho katika Vijiji

Maeneo ya malisho ndani ya vijiji yatapatikana kwa njia zifuatazo:-

a) Maeneo ya malisho yanayomilikiwa na mfugaji mmoja mmoja (individual owned grazing land). Maeneo haya hupatikana kwa mfugaji kununua eneo lake binafsi au kurithi kutoka katika familia.

b) Maeneo ya malisho ya jamii ya wafugaji yanayomilikiwa kwa pamoja (communal grazing land). Maeneo haya hupatika kwa njia zifuatazo:-

(i) Maeneo yaliyoainishwa na kutengwa kupitia Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Sura Na.114 na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Sura Na.116.

(ii) Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho katika vijiji ambavyo havijafanya Mpango wa Matumizi ya Ardhi.

### 2.1.1 Majukumu muhimu ngazi ya Halmashauri

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ataunda Kamati ya uhamasishaji wa upatikanaji wa maeneo ya malisho na itajumuisha wajumbe wafuataO:-

a) Mtaalam kutoka Idara inayosimamia Mifugo na Uvuvi,
b) Mtaalam kutoka Idara inayosimamia Kilimo
c) Mtaalam kutoka Idara inayosimamia Ardhi
d) Mtaalam kutoka Idara inayosimamia Maliasili
e) Mtaalam kutoka Idara inayosimamia Maendeleo ya Jamii
f) Mtaalam kutoka Idara inayosimamia Maji

Kamati hiyo itafanya kazi ya kuhamasisha na kushawishi vijiji viweze kutenga maeneo kwa ajili ya malisho. Baada ya Kamati hiyo kukamilisha zoezi la uhamasishaji wa utengaji wa maeneo ya malisho, itapeleka taarifa kuhusu mafanikio ya zoezi hilo kwa

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Baada ya kupokea taarifa ya Kamati ya uhamasishaji wa utengaji wa maeneo ya malisho Mkurugenzi ataagiza na kuisimamia Kamati ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya (Participatory Land Use Management Team - PLUM) izingatie ushauri wa Kamati ya uhamasishaji wakati wa kutekeleza zoezi la mpango wa matumizi ya ardhi utakaotenga eneo la malisho.

### 2.1.2 Majukumu muhimu ngazi ya Kijiji

a) Halmashauri ya kijiji itaainisha na kuchagua maeneo ya malisho yanayofaa kutokana na taarifa zilizopo au kutokana na umuhimu wa maeneo hayo kwa wafugaji waliopo na idadi ya mifugo iliyopo;

b) PLUM itakutana na Serikali ya Kijiji na kutambulisha dhana na misingi ya mpango wa matumizi ya ardhi ili kufanikisha upatikanaji wa maeneo ya malisho pamoja na kuelezea hatua za kubainisha na kutenga maeneo;

c) Halmashauri ya Kijiji itaitisha Mkutano Mkuu maalum wa Kijiji kwa ajili ya kutambulisha dhana na misingi ya mpango wa matumizi ya ardhi kwa lengo la kufanikisha upatikanaji wa maeneo ya malisho pamoja na kuelezea hatua za kubainisha na kutenga maeneo;

d) Serikali ya Kijiji itaunda na kuelekeza Kamati ya Usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kijiji (Village Land Use Management – VLUM) kushirikiana na PLUM katika shughuli nzima ya ubainishaji na utengaji wa maeneo;

e) PLUM itatoa elimu kwa VLUM na kuelezea faida na hatua zitakazochukuliwa katika utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi ambao utatenga eneo la malisho;

f) PLUM na VLUM zitazungukia mipaka yote ya Kijiji na kubainisha rasilimali zote zilizopo kwenye ardhi na kurekodi alama zote za mipaka (mf: mito, barabara kubwa, miamba na miti mikubwa);

g) VLUM itashirikiana na PLUM kutekeleza upimaji, uchoraji na uwekaji wa alama kwenye maeneo ya mpango wa matumizi ya ardhi yakiwemo maeneo ya malisho;

h) PLUM na VLUM watawasilisha kwenye Mkutano Mkuu maalum wa Kijiji mapendekezo ya mpango wa matumizi ya ardhi kwa kuzingatia shughuli za kiuchumi zilizopo kijijini kwa lengo la kuupitisha mpango huo.

### 2.1.3 Uundwaji wa Kamati ya Usimamizi wa Malisho ya Kijiji

Mambo yafuatayo yatazingatiwa baada ya maeneo ya malisho kupatikana:-

a) Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji ngazi ya Kijiji kwa kushirikiana na Serikali ya Kijiji ataitisha Mkutano wa wafugaji kwa ajili ya kuwatambua wafugaji waliopo, idadi ya mifugo walionayo na kuwaorodhesha kwenye daftari maalum kwa ajili ya kumbukumbu;

b) Katika mkutano huo wafugaji watahamasishwa kujiunga kwenye ushirika au vikundi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma zinazohusiana na uendelezaji wa maeneo ya malisho na ufugaji wenye tija. Vile vile, elimu ya mahusiano

itatolewa kwa wafugaji, viongozi na wajumbe wa Serikali ya Kijiji;

c) Ushirika au vikundi vya wafugaji vitakaoundwa vitachagua viongozi ambao wataunda Kamati ya Usimamizi wa Malisho ya Kijiji. Viongozi watakaochaguliwa ni Mwenyekiti na Mtunza Hazina. Katibu wa Kamati atakuwa ni Afisa Mifugo anayesimamia kijiji husika na wajumbe wengine watakuwa ni Mwenyekiti wa timu ya mipango ya matumizi ya ardhi ya kijiji (VLUM) na mjumbe mmoja kutoka Chama cha Wafugaji ngazi ya Kijiji.

### 2.1.4 Majukumu ya Kamati ya Usimamizi wa Malisho ya kijiji

a) Kuwasimamia wafugaji kutekeleza wajibu na majukumu yao kwenye maeneo ya malisho;

b) Kutunga Kanuni na Taratibu za kusimamia na kuendeleza maeneo ya malisho;

c) Kuhamasisha wafugaji kuchangia fedha kwa ajili ya kupima, kuweka alama zinazoonekana, kuchora ramani ya eneo lililotengwa kwa ajili ya malisho;

d) Kushirikiana na wataalam kupima, kuweka alama zinazoonekana, kuchora ramani ya eneo lililotengwa kwa ajili ya malisho;


e) Baada ya upimaji wa eneo la malisho, Katibu wa Kamati atawasilisha nyaraka husika za upimaji kwenye Serikali ya Kijiji na kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kwa hatua ya kuziwasilisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kusajili na kutangaza eneo hilo kwenye Gazeti la Serikali.

### 2.1.5 Wajibu na majukumu ya wafugaji katika kutunza na kuendeleza eneo la malisho la kijiji

a) Kuandaa mpango kina wa eneo la malisho (Detailed grazing land management plan) kwa kushirikiana na Mkaguzi wa Maeneo ya Malisho wa eneo husika;

b) Miaka miwili (2) baada ya eneo la malisho kupatikana, wafugaji wana wajibu wa kupunguza vichaka ili kuruhusu uotaji wa malisho, kuotesha malisho mapya (reseeding) na miti malisho kwenye sehemu zisizo na malisho;




***Picha Na 1. Uondoaji wa vichaka kwenye eneo la malisho huwezesha malisho kuota na kustawi vizuri***

c) Kushirikiana na Serikali kujenga na kukarabati miundombinu ya mifugo kama visima virefu, mabwawa/malambo, mabirika/mbauti, vibanio na majosho;

d) Kutunza mazingira ya maeneo ya malisho na vyanzo vya maji, kwa kufuata taratibu za Sheria Na.11 ya Mwaka 2009 ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimaji za Maji;

e) Wafugaji watawajibika kuzuia uchomaji moto holela kwenye maeneo ya malisho kwa kuweka ulinzi, barabara za kuzuia moto, nk ili kutoharibu uoto wa malisho;



***Picha Na 2. Madhara ya uchomaji moto holela huharibu uoto wa malisho***

f) Kuzuia mmomonyoko wa udongo kwa kutumia njia mbalimbali mfano makinga maji, kupanda miti malisho na nyasi;

g) Miaka miwili (2) baada ya eneo la malisho kupatikana, wafugaji wana wajibu wa kuondoa magugu sumbufu na vamizi kwenye eneo la malisho;

h) Kulisha mifugo kwa mfumo wa kuzunguka (*rotational grazing*) ili kuzuia mmomonyoko na kuruhusu malisho kuota na kustawi vizuri;

i) Kutenga eneo lisilopungua asilimia 10 ya eneo lote la malisho lililotengwa ili kuanzisha shamba la malisho mapya kwa lengo la kuvuna malisho na mbegu (*pasture establishment)*;

j) Wafugaji kwa kushirikiana na wataalam wa malisho watatathmini uwezo wa eneo la malisho (carrying capacity) kwa kubaini idadi ya mifugo itakayotumia eneo husika, na kuhakikisha uwepo wa idadi ya mifugo inayolingana na uwezo wa eneo la malisho lililotengwa kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Maeneo ya

Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura Na. 180 kifungu Na. 20 (1);



***Picha Na. 3. Eneo la malisho ambalo halikuzingatia idadi ya mifugo na uwezo wa eneo***

k) Kutoa taarifa mbalimbali za eneo la malisho pamoja na mifugo kwa mamlaka husika;

l) Kulinda eneo la malisho lisivamiwe na watumiaji wengine wa ardhi na kutofanya shughuli yoyote tofauti na ufugaji.

**2.1.6 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri katika kutunza na kuendeleza eneo la malisho la kijiji**

Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri nchini zinawajibu wa kutekeleza mwongozo huu kwa kufanya yafuatayo:-

a) Kutenga fedha kwa ajili ya kuwezesha uandaaji na mapitio ya mipango ya matumizi ya ardhi za vijiji;

b) Kutenga na kutumia asilimia 15 ya mapato yatokanayo na mifugo (Waraka wa Rais Na.1 wa Mwaka 2002) kwa lengo la kujenga na kukarabati miundombinu ya mifugo (majosho, mabwawa, visima virefu, minada na vibanio);

c) Kuandaa, kusimamia na kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi za vijiji;

d) Kusimamia uandaaji wa mpango kina wa eneo la malisho (Detailed grazing land management plan) kwa kushirikiana na wafugaji wa eneo husika;

e) Kusimamia matumizi sahihi ya maeneo ya malisho yaliyotengwa ikiwemo upunguzaji wa vichaka, uoteshaji malisho na miti malisho, uondoaji magugu vamizi/sumbufu pamoja na kuhakikisha uwepo wa Idadi ya mifugo kulingana na uwezo wa eneo;



***Picha Na. 4. Eneo la malisho lililooteshwa malisho aina ya nyasi***

f) Kushirikiana na wadau wengine kutoa elimu kuhusu upandaji, uvunaji, uhifadhi na matumizi sahihi ya malisho na mbegu za malisho;

g) Kuhakikisha upatikanaji wa mbegu za malisho kwa ajili ya kuboresha maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho.




*Picha Na. 5. Malisho yaliyooteshwa kwa lengo la kuvuna mbegu za malisho*

**2.1.7 Majukumu ya Wizara katika kutunza na kuendeleza eneo la malisho la kijiji**

a) Kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri pamoja na wadau wengine katika jukumu la kutenga, kupima na kuweka alama za mipaka zinazoonekana kwenye maeneo ya malisho;

b) Kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri pamoja na wadau wengine kujenga na kukarabati miundombinu ya mifugo (majosho, mabwawa, visima virefu, minada na vibanio);

c) Kusajili na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali maeneo ya malisho yaliyotengwa ili kuyalinda kisheria;

d) Kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri pamoja na wadau wengine kutoa elimu kuhusu upandaji, uvunaji, uhifadhi na matumizi sahihi ya malisho na mbegu za malisho;

e) Kuteuwa Wakaguzi wa Maeneo ya Malisho na kuwasimamia kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri husika;

f) Kuhakikisha upatikanaji wa mbegu za malisho kwa ajili ya kuboresha maeneo yaliyotengwa.

## 2.2 Utaratibu wa Upatikanaji wa Maeneo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Ngazi ya Halmashauri

Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri zenye maeneo zinahamasishwa kuyatenga, kuyagawa katika vitalu vya ufugaji (block Farming) na kuwapangisha wafugaji. Hii itasaidia kuongeza maeneo ya malisho na kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi inayotokana na uhaba wa maeneo ya malisho. Vile vile, utengaji huo wa maeneo ya malisho utahamasisha uwekezaji katika Sekta ya Mifugo.

### 2.2.1 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ataunda Kamati ya uhamasishaji wa upatikanaji wa maeneo ya malisho ambayo itajumuisha wajumbe wafuatao: -

a) Mkuu wa Idara ya mifugo kutoka Halmashauri husika
b) Afisa mipango miji na Vijiji wa Halmashauri husika
c) Mwakilishi wa Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi
d) Afisa Ardhi kutoka Halmashauri husika
e) Afisa Mifugo kutoka Halmashauri husika

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri atateua Mwenyekiti wa Kamati hiyo na Katibu atakuwa Afisa Mifugo kutoka Halmashauri husika.

### 2.2.2 Majukumu ya Kamati ya uhamasishaji wa upatikanaji wa maeneo ya malisho

a) Kufanya vikao vya kutafuta na kuhamasisha upatikanaji wa maeneo ya malisho kwenye Halmashauri husika;

b) Baada ya maeneo kupatikana Kamati itawasilisha kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri mahitaji ya fedha kwa ajili ya utengaji na upimaji wa vitalu ambavyo vitatumika kwa utaratibu maalum wa kupangisha. Utengaji huo wa vitalu utaiwezesha Halmashauri kukusanya mapato kutokana na kodi itakayotozwa;

c) Kamati itasimamia zoezi la upimaji wa eneo la malisho lililoainishwa na kuweka mawe ya mipaka (beacons);

d) Kamati itasimamia utengaji wa vitalu kulingana na ukubwa wa eneo. Kitalu kinaweza kuwa na ukubwa wa kuanzia Ha. 200 sawa na ekari 500 na kuendelea.

### 2.2.3 Utaratibu wa upangishaji wa vitalu

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri atatoa tangazo la upangishaji wa vitalu litakalobainisha utaratibu utakaofuatwa na mwombaji katika kutuma maombi. Utaratibu huo utajumuisha mambo yafuatayo:-

a) Barua ya maombi kwenda kwa Mkurugenzi kupitia kwa Mwenyekiti wa Kijiji/Serikali ya mtaa na Mtendaji wa Kata. Barua hiyo itatakiwa kuwa na viambatisho ambavyo ni nakala ya kitambulisho cha Taifa/kitambulisho cha mpiga kura/Hati ya kusafiria, nakala ya cheti cha kuzaliwa vilivyothibitishwa na Mwanasheria, barua ya kuonesha uthibitisho wa umiliki wa mifugo kutoka Serikali za Mtaa/Kijiji na stakabadhi halisi ya

malipo kwa ajili ya maombi. Aidha, wanaotoka nje ya kijiji/mtaa/kata husika aambatishe cheti cha tabia njema kutoka kituo cha Polisi;

b) Mwombaji anatakiwa kulipa kiasi cha fedha kisichozidi shilingi 50,000 kama ada ya maombi ambayo haitarudishwa baada ya malipo kufanyika;

c) Tangazo la upangishaji wa vitalu litaainisha gharama ya kupangisha vitalu husika. Gharama ya upangishaji itakuwa shilingi 3,500 kwa ekari moja kwa mwaka. (Gharama hii itabadilika baada ya Wizara kufanya marejeo ya bei ya upangishaji wa vitalu);

d) Halmashauri itaandika barua kwa ajili ya kujibu maombi ya mfugaji kama yamekubaliwa au yamekataliwa;

e) Endapo maombi ya mfugaji yamekubaliwa mfugaji ataoneshwa kitalu na kupewa utaratibu wa kufanya malipo;

f) Mfugaji atasaini Mkataba wa ukodishaji kitalu utakaoandaliwa na Halmashauri husika kabla hajakabidhiwa kitalu;

g) Baada ya mfugaji kukamilisha taratibu za malipo na kusaini Mkataba atakabidhiwa kitalu.

### 2.2.4 Majukumu ya mfugaji baada ya kupangishwa kitalu

Baada ya mfugaji kupangishwa kitalu pamoja na masharti mengine yaliyoainishwa kwenye mkataba atatakiwa kutekeleza majukumu yaliyoainishwa kwenye Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1. Majukumu ya mfugaji**

| Na. | Jukumu | Muda wa utekelezaji |
|---|---|---|
| 1 | Kupunguza vichaka (Bush clearing) kwa asilimia isiyopungua 15 ya ukubwa wa kitalu alichopangishwa kwa mwaka ili kuruhusu uotaji wa malisho na kuotesha malisho mapya kwenye sehemu zisizo na malisho (reseeding) | Mwaka mmoja baada ya kupangishwa na kuendelea kila mwaka mpaka kukamilisha eneo lote la kitalu. |
| 2 | Kuzuia uchomaji moto holela kwenye kitalu | Muda wote wa upangishwaji |
| 3 | Ulimaji na upandaji wa malisho mapya na miti malisho kwenye asilimia 25 ya eneo lote la kitalu kwa kuanza na eneo la asilimia 6.25 | Mwaka mmoja baada ya kupangishwa na kuendelea kila mwaka mpaka kukamilisha asilimia 25 ya eneo lote la kitalu. |
| 4 | Kuondoa magugu sumbufu/vamizi kwenye kitalu | Muda wote wa upangishwaji |
| 5 | Kulisha mifugo kwa mfumo wa kuzunguka (rotational grazing) ili kuruhusu malisho kuota na kustawi vizuri. | Muda wote wa upangishwaji |


| Na. | Jukumu | Muda wa utekelezaji |
|---|---|---|
| 6 | Pamoja na masharti mengine yaliyoainishwa kwenye Mkataba mfugaji atatakiwa kulinda eneo la kitalu alilopangishwa lisivamiwe na watumiaji wengine wa ardhi na kulitumia kwa ajili ya ufugaji na si vinginevyo | Muda wote wa upangishwaji |
| 7 | Kuzuia mmomonyoko wa udongo kwa kutumia njia mbalimbali mfano makinga maji, kupanda malisho n.k | Muda wote wa upangishwaji |
| 8 | Kutunza miundombinu ya maji iliyopo kwenye kitalu na kutunza mazingira | Muda wote wa upangishwaji |
| 9 | Kujenga miundombinu ya josho, maji, kibanio n.k | Muda wote wa upangishwaji |

**Angalizo**: Mkaguzi wa Maeneo ya Malisho atakagua na kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya mfugaji baada ya kukabidhiwa kitalu katika kila robo ya mwaka. Idadi ya uniti za mifugo kwenye kitalu itazingatia uwiano kama ilivyoelekezwa kwenye jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2 Makadirio ya idadi ya uniti za mifugo kwa ukubwa wa kitalu ambacho hakijaendelezwa**

| Na. | Aina ya kitalu | Ukubwa wa kitalu (Ha) | Makisio ya idadi ya uniti za mifugo |
|---|---|---|---|
| | Kidogo | 200 | 100 - 140 |
| | Kati | 201 - 400 | 140 - 270 |
| | Kikubwa | 401 - 600 | 270 - 400 |

**Angalizo:** Idadi ya mifugo kwenye kitalu itaongezeka baada ya kushauriwa na Mkaguzi wa Maeneo ya Malisho kutokana na uendelezaji utakaofanyika



***Picha Na. 6. Mifugo inayolishwa kwa mfumo wa mzunguko (rotational grazing) katika kitalu ili kuruhusu malisho kuota na kustawi vizuri***

### 2.2.5 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri kwenye maeneo ya vitalu

a) Kuanzisha mashamba darasa ya malisho kwenye vitalu vilivyotengwa kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili wafugaji waweze kujifunza kuhusu kilimo cha malisho;

b) Kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu uboreshaji wa koosafu, uvunaji wa mifugo, uvunaji wa maji na udhibiti wa magonjwa ya mifugo;

c) Kuwasimamia wafugaji na kuhakikisha kuwa wanatunza na kuendeleza vitalu kwa kupanda malisho;

d) Kuwasimamia wafugaji na kuhakikisha kuwa wanafuga mifugo kulingana na uwezo wa kitalu;

e) Kuhakikisha maeneo yote ya vitalu yanakaguliwa na Mkaguzi wa Maeneo ya Malisho na kutolewa taarifa katika kila robo ya mwaka;

f) Kuhakikisha kuwa maeneo ya vitalu hayatumiki kwa shughuli nyingine yoyote isipokuwa ufugaji.

### 2.2.6 Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye maeneo ya vitalu

a) Kuhamasisha uanzishaji wa mashamba darasa ya malisho kwenye vitalu vilivyotengwa kwa kushirikiana na Halmashauri ili wafugaji waweze kujifunza kuhusu kilimo cha malisho;

b) Kushirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri kuwasimamia Wakaguzi wa Maeneo ya Malisho;

c) Kushirikiana na Halmashauri kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu ufugaji wenye tija.

### 2.2.7 Mchanganuo na idadi ya vitalu

Halmashauri ya Wilaya itaandaa mchanganuo na idadi ya vitalu vilivyopo kwa ajili ya kumbukumbu. **Kiambatisho Na.1**

## 2.3 Utaratibu wa Upatikanaji wa Maeneo Yaliyoainishwa na Taasisi za Serikali

Wizara kwa kushirikiana na Taasisi husika itatambua na kutenga maeneo ambayo hayatumiki lakini yanafaa kwa ufugaji kwa lengo la kukodisha kwa wafugaji. Wizara kwa kushirikiana na Taasisi husika itaunda timu ya upimaji ambayo itajumuisha wataalam kutoka Wizara za Mifugo na Uvuvi, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Taasisi husika na Mtaalamu wa Mifugo kutoka Halmashauri husika.

Hatua zifuatazo zitahusika:-

a) Kuitisha mkutano wa Halmashauri za Serikali za vijiji vinavyozunguka eneo husika kwa ajili ya kuelezea kusudio la upimaji au utengaji wa maeneo ya kuwakodishia wafugaji;

b) Taasisi ya Serikali kwa kushirikiana na Timu ya upimaji zitaainisha na kutenga maeneo yaliyopendekezwa ili yaweze kupangishwa kwa wafugaji. Maeneo yanayomilikiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo yamepunguza matumizi yake yatamegwa na kutengwa kwa ajili ya Wafugaji kwa utaratibu wa kupangishwa ambapo Wizara itaendelea kuwa mmiliki wa maeneo hayo;

c) Timu ya upimaji itaendesha zoezi la uhakiki wa maeneo kwa njia shirikishi na kutembelea maeneo yote kwa pamoja na kuchukua majira nukta (coordinates) ya eneo husika. Afisa Mpima Ardhi atachora ramani ya eneo husika na kutenga vitalu katika eneo hilo kutokana na ukubwa wa eneo na kuwasilisha michoro kwa ajili ya kuandaa ramani.

### 2.3.1 Utaratibu wa upangishaji wa kitalu

Taasisi itatoa tangazo la upangishaji wa vitalu ambalo litabainisha utaratibu utakaofuatwa na mwombaji katika kutuma maombi. Utaratibu huo utajumuisha mambo yafuatayo:-

a) Barua ya maombi kwenda kwa Mkuu wa Taasisi kupitia kwa Mwenyekiti wa Kijiji/Serikali ya mtaa, Mtendaji wa Kata na Cheti cha tabia njema kutoka kituo cha Polisi. Barua hiyo itatakiwa kuwa na viambatisho ambavyo ni nakala ya kitambulisho cha Taifa/kitambulisho cha mpiga kura/Hati ya kusafiria, nakala ya cheti cha kuzaliwa vilivyothibitishwa na Mwanasheria, barua ya kuonesha uthibitisho wa umiliki wa mifugo kutoka Serikali za mtaa/Kijiji na stakabadhi halisi ya malipo kwa ajili ya maombi;

b) Mwombaji anatakiwa kulipa kiasi cha fedha zisizozidi shilingi 50,000 kama ada ya maombi ambayo haitarudishwa baada ya malipo kufanyika;

c) Tangazo la upangishaji wa vitalu litaainisha gharama ya kupangisha vitalu husika. Gharama ya upangishaji itakuwa shilingi 3,500 kwa ekari moja kwa mwaka. (Gharama hii itabadilika baada ya Wizara kufanya marejeo ya bei ya upangishaji wa vitalu);

d) Taasisi itaandika barua kwa ajili ya kujibu maombi ya mfugaji kama yamekubaliwa au yamekataliwa;

e) Endapo maombi ya mfugaji yamekubaliwa mfugaji ataoneshwa kitalu na kupewa utaratibu wa kufanya malipo;

f) Mfugaji atasaini Mkataba wa ukodishaji kitalu utakao andaliwa na Taasisi husika kabla hajakabidhiwa kitalu;

g) Baada ya mfugaji kukamilisha taratibu za malipo na kusaini Mkataba atakabidhiwa kitalu.

### 2.3.2 Majukumu ya mfugaji baada ya kukabidhiwa kitalu

Baada ya mfugaji kupangishwa kitalu pamoja na masharti mengine yaliyoainishwa kwenye mkataba atatakiwa kutekeleza majukumu yaliyoainishwa kwenye Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Majukumu ya Mfugaji**

| Na. | Jukumu | Muda wa utekelezaji |
|---|---|---|
| 1 | Kupunguza vichaka (Bush clearing) kwa asilimia isiyopungua 15 ya kitalu alichopangishwa kwa mwaka ili kuruhusu uotaji wa malisho na kuotesha malisho mapya kwenye sehemu zisizo na malisho (reseeding) | Mwaka mmoja baada ya kupangishwa na kuendelea kila mwaka mpaka kukamilisha eneo lote la kitalu. |
| 2 | Kuzuia uchomaji moto holela kwenye kitalu | Muda wote wa upangishwaji |
| 3 | Ulimaji na upandaji wa malisho mapya na miti malisho kwenye asilimia 25 ya eneo lote la kitalu kwa kuanza na eneo la asilimia 6.25 | Mwaka mmoja baada ya kupangishwa na kuendelea kila mwaka mpaka kukamilisha asilimia 25 ya eneo lote la kitalu. |
| 4 | Kuondoa magugu sumbufu/vamizi kwenye | Muda wote wa upangishwaji |

| Na. | Jukumu | Muda wa utekelezaji |
|---|---|---|
| | kitalu | |
| 5 | Kulisha mifugo kwa mfumo wa kuzunguka (rotational grazing) ili kuruhusu malisho kuota na kustawi vizuri. | Muda wote wa upangishwaji |
| 6 | Pamoja na masharti mengine yaliyoainishwa kwenye Mkataba mfugaji atatakiwa kulinda eneo la kitalu alilopangishwa lisivamiwe na watumiaji wengine wa ardhi na kulitumia kwa ajili ya ufugaji na si vinginevyo | Muda wote wa upangishwaji |
| 7 | Kuzuia mmomonyoko wa udongo kwa kutumia njia mbalimbali mfano makinga maji, kupanda malisho n.k | Muda wote wa upangishwaji |
| 8 | Kutunza miundombinu ya maji iliyopo kwenye kitalu na kutunza mazingira | Muda wote wa upangishwaji |
| 9 | Kujenga miundombinu ya josho, maji, kibanio n.k | Muda wote wa upangishwaji |

**Angalizo**: Vitalu vilivyokodishwa kwa wafugaji vitakaguliwa na Taasisi husika kwa kumhusisha Mkaguzi wa Maeneo ya Malisho juu ya uendelezaji na kutolewa taarifa kila robo ya mwaka. Idadi ya uniti za mifugo kwenye kitalu itazingatia uwiano kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 2.

### 2.3.3 Majukumu ya Taasisi kwenye maeneo ya vitalu

a) Kuanzisha mashamba darasa ya malisho kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili wafugaji waweze kujifunza kuhusu kilimo cha malisho uvunaji na uhifadhi;

b) Kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu uboreshaji wa koosafu; uvunaji wa mifugo; uvunaji wa maji na udhibiti wa magonjwa ya mifugo;

c) Kuwasimamia wafugaji na kuhakikisha kuwa wanatunza na kuendeleza vitalu kwa kupanda malisho;

d) Kuwasimamia wafugaji na kuhakikisha kuwa wanafuga mifugo kulingana na uwezo wa kitalu;

e) Kuhakikisha maeneo yote ya vitalu yanakaguliwa na Mkaguzi wa Maeneo ya Malisho na kutolewa taarifa katika kila robo ya mwaka;

f) Kuhakikisha kuwa maeneo ya vitalu hayatumiki kwa shughuli nyingine yoyote isipokuwa ufugaji.

### 2.3.4 Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye maeneo ya vitalu kutoka kwenye mashamba ya Taasisi

a) Kushirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri husika kuwasimamia Wakaguzi wa maeneo ya malisho wakague maeneo ya malisho ya taasisi husika.

b) Kushirikiana na Taasis kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu ufugaji wenye tija.

### 2.3.5 Mchanganuo na Idadi ya Vitalu

Taasisi itaandaa mchanganuo na idadi ya vitalu vilivyopo kwa lengo la kutunza kumbukumbu. **Kiambatisho Na.2**

# SURA YA TATU

## 3.0 UMILIKI WA MAENEO YA MALISHO

Maeneo ya malisho yaliyoainishwa, kutengwa, kupimwa na kuwekewa alama zinazoonekana yatasajiliwa na Mkurugenzi wa Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo kwa mujibu wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura Na 180.

Maeneo ya malisho yaliyopatikana yatatangazwa kwenye Gazeti la Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura Na. 180 Kifungu cha 16 kwa lengo la kuyalinda ili yasivamiwe na watumiaji wengine wa ardhi.

Maeneo ya malisho yaliyotengwa na kuwekewa alama za mipaka yatamilikishwa kwa mujibu wa sheria ambapo;

a) Maeneo yaliyopatikana katika ardhi ya kijiji yatamilikishwa kwa hati miliki ya kimila (Customary Certificate Right of Occupancy -CCROs),
b) Maeneo yaliyopatikana katika ardhi ya jumla yatamilikishwa kwa hati miliki ya kupewa na Serikali (Granted right of Occupancy- GRO) na
c) Maeneo yaliyopatikana katika ardhi za hifadhi umilikishwaji wake utategemea ardhi hiyo iko katika kundi gani kati ya ardhi ya kijiji au ardhi ya jumla.

**Angalizo**:

Kwa eneo la malisho linalopakana na vijiji zaidi ya kimoja na wamiliki wamekubaliana kulitumia kwa pamoja, eneo hilo litasimamiwa na kutumiwa kwa pamoja kama eneo la malisho la vijiji vyote vilivyopakana. Eneo hilo litatumiwa na wafugaji wa vijiji vilivyoungana kwa makubaliano ya pande zote kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Sura Na.114 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Sura Na.116. Kamati ya pamoja inayohusisha wajumbe wa Kamati za vijiji zinazoshughulikia ardhi watatembelea eneo la malisho na kubaini mipaka ya kila eneo la malisho la kijiji husika. Uhakiki wa eneo la malisho la kijiji utawekwa bayana kwenye ramani na kwa kuchukuliwa majira nukta (coordinates) kwa GPS.

Hati miliki zitakazotolewa za maeneo ya malisho zitakabidhiwa kwa Ushirika/Chama/Vikundi au Wafugaji binafsi waliolengwa.

Ushirika/Chama/Vikundi ni muhimu sana katika kulinda, kutunza na kuendeleza eneo la malisho kwa mujibu wa mpango kina wa matumizi wa eneo hilo (Detailed grazing land management plan).

Ushirika unaotarajiwa katka maeneo ya malisho utaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Sura Na. 337, Chama kitaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Vyama na kikundi kitaundwa kwa mujibu wa sheria za usimamizi wa vikundi vya kijamii chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Afisa Maendeleo ya Jamii (W) atashirki kutoa elimu ya uundaji wa vikundi).

### 3.1 Faida za Umiliki wa Maeneo ya Malisho

a) Upatikanaji wa uhakika wa malisho na maji

Kupatikana kwa maeneo ya malisho kutawawezesha wafugaji kuwa na eneo la uhakika la kupanda na kuboresha malisho kwa ajili ya mifugo kwa kipindi chote cha mwaka hivyo kukidhi viwango na hitaji la soko kwa muda mfupi na kuongeza tija na kipato kwa mfugaji pamoja na kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo na kuchangia katika pato la Taifa.

b) Umilikishaji wa maeneo utaboresha na kupanua soko la Malisho na Mbegu za Malisho. Upatikanaji wa mbegu za malisho pamoja na malisho yenyewe uko chini kwa sasa, umilikishaji wa maeneo kwa Ushirika/Chama/Vikundi utachochea mwamko wa uzalishaji wa mbegu na uhitaji wa malighafi (mbegu na malisho) kwa ajili ya ufugaji bora.

c) Umilikishaji wa maeneo kwa Ushirika/Chama/Vikundi utachochea kuanzishwa kwa mpango wa kopa mbegu lipa mbegu na utawezesha kuongezeka kwa upatikanaji na matumizi ya pembejeo za mifugo.

d) Umilikishaji wa maeneo utaboresha uwekaji sahihi wa takwimu za maeneo ya malisho nchini.

e) Umilikishwaji wa maeneo ya malisho utapunguza uvamizi wa maeneo ya malisho na utasaidia kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

f) Umilikishwaji wa maeneo ya malisho utasaidia kuwafanya wafugaji waaminike kwa Taasisi za kifedha na hivyo kuaminiwa kupewa mikopo.

# SURA YA NNE

## 4.0 USIMAMIZI NA MATUMIZI ENDELEVU YA MAENEO YA MALISHO

Usimamizi na utekelezaji wa Mwogozo huu utakuwa chini ya Wizara za Mifugo na Uvuvi, OR-TAMISEMI pamoja na wadau wengine. Hivyo, wataalam wakiwemo Maafisa Mifugo na Wakaguzi wa Maeneo ya Malisho katika wizara hizo watahusika katika kutenga, kupima, kumilikisha na kusimamia Wafugaji na Wadau wengine kwa nia ya kuongeza maeneo ya ufugaji na maeneo ya malisho yaliyopimwa ili kufikia lengo la upatikanaji wa uhakika wa malisho na maji kwa mifugo.

Maeneo ya malisho ni sharti yaendelezwe kwa kupandwa malisho yanayoendana na ukanda wa kiikolojia wa eneo husika pamoja na hali ya hewa ya eneo hilo. Malisho hustawi vizuri iwapo yamepandwa katika eneo ambalo mazingira yanalingana na mahitaji ya aina ya malisho husika. Kwa hivyo ni vyema wakati wa kuchagua malisho ya kupanda kuoanisha aina ya malisho na mazingira yaliyopo.

Malisho yanayotakiwa kupandwa hapa Tanzania ni ya aina nyingi, ikiwepo ya asili na ya kigeni. Nchi ya Tanzania ni kubwa yenye maeneo yanayotofautiana katika aina, rutuba, kiasi cha alkali (base) au tindikali (acid) katika udongo, hali ya hewa (kiasi cha mvua na nyuzi joto), mwinuko kutoka usawa wa bahari, mteremko au tambarare n.k. Kwa mantiki hiyo, mwongozo huu utamsaidia mmiliki wa eneo la malisho kuoanisha aina ya malisho na mahali panapofaa kupandwa malisho hayo.

Ili kurahisisha zoezi la uchaguzi wa malisho ya kupanda, Tanzania imegawanywa katika kanda kuu saba za hali ya hewa kama ilivyooneshwa katika **kiambatisho Na. 3.**

Tija katika ufugaji hutegemea moja kwa moja utunzaji wa malisho na maeneo ya malisho. Wafugaji wengi wanaotumia maeneo ya malisho ya pamoja (communal grazing land) wameshindwa kutunza, kusimamia na kuendeleza maeneo hayo na kusababisha uharibifu wa ardhi na ukosefu wa malisho. Hii inatokana na vijiji kutokuwa na mkakati endelevu wa kuboresha na kutunza maeneo ya malisho yaliyotengwa. Hivyo basi, uendelezaji wa maeneo ya malisho ni muhimu kwa kuwa utawezesha upatikanaji wa uhakika wa malisho na maji kwa mifugo. Jukumu la uendelezaji wa maeneo ya malisho litafanywa na wafugaji wa eneo husika.

### 4.1 Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho

a) Wafugaji wana wajibu wa kupunguza vichaka ili kuruhusu uotaji wa malisho, kuotesha malisho mapya (reseeding) na miti malisho kwenye sehemu zisizo na malisho;

b) Wafugaji wana wajibu wa kujenga, kukarabati na kuilinda miundombinu ya mifugo kama visima virefu, mabwawa, mabirika/mbauti, vibanio na majosho;

c) Kutunza mazingira ya maeneo ya malisho na vyanzo vya maji;

d) Wafugaji wanawajibika kuzuia uchomaji moto holela kwenye maeneo ya malisho;

e) Wafugaji wana wajibu wa kuanzisha shamba la malisho mapya (*pasture establishment*) kwa lengo la kuvuna malisho na mbegu;

f) Wafugaji wana wajibu wa kuondoa magugu sumbufu na vamizi kwenye maeneo ya malisho;

g) Wafugaji wana wajibu wa kulisha mifugo kwa mfumo wa kuzunguka (*rotational grazing*) ili kuzuia mmomonyoko wa udongo na kuruhusu malisho kuota na kustawi vizuri;

h) Wafugaji wana wajibu wa kulisha mifugo kulingana na uwezo wa eneo lililotengwa.

## 4.2 Usimamizi wa Maeneo ya Malisho

Maeneo ya malisho yatatumika kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura Na. 180. Sheria inaelekeza mambo yafuatayo: -

a) Wamiliki (wafugaji) walinde maeneo ya malisho.

b) Hairuhusiwi kufanyika kwa shughuli nyingine tofauti na ufugaji kama vile uanzishaji wa makazi, kilimo, uchimbaji wa madini na uanzishaji wa hifadhi za wanyama pori ndani ya eneo la malisho.

c) Wafugaji watasimika mabango pande zote nne yenye urefu wa mita tatu kwenda juu yanayosomeka kutoka umbali wa mita mia moja na kuainisha shughuli zisizoruhusiwa kufanyika katika eneo la malisho.

d) Wafugaji kwa kushirikiana na Wataalam wa Mifugo na Wakaguzi wa Maeneo ya Malisho waandae mpango

wa uvunaji wa mifugo kwa kila mwaka pale ambapo idadi ya mifugo itazidi uwezo wa eneo la malisho lililotengwa.

e) Kila eneo lililotengwa kwa ajili ya malisho litakaguliwa na Mtaalam wa Mifugo/Mkaguzi wa Maeneo ya Malisho na atashirikiana na kamati husika kusimamia matumizi sahihi ya eneo la malisho.

### 4.3 Kamati za Usimamizi wa Maeneo ya Malisho

Kwa Mujibu wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za vyakula vya Wanyama Sura Na. 180 inaelekeza kuwepo kwa Baraza la Ushauri wa Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama katika ngazi ya Kitaifa. Pamoja na majukumu mengine, Baraza litahamasisha kuanzishwa kwa kamati za usimamizi wa maeneo ya malisho katika ngazi ya Halmashauri, Kata na Kijiji.

a) Baraza la Taifa la Ushauri wa Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama
   (i) Baraza litashirikiana na Idara ya Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo (DGLF) kulinda na kuwa na usimamizi endelevu wa maeneo ya malisho.
   (ii) Majukumu ya Baraza ni pamoja na kushauri kuhusu sera na mikakati ya uhamasishaji, uendelezaji na usimamizi wa maeneo ya malisho.

b) Kamati ya Usimamizi wa Maeneo ya Malisho katika ngazi ya Wilaya

Mwenyekiti wa Kamati hii atakuwa Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi, katibu atakuwa Mkaguzi wa Maeneo ya Malisho ngazi ya Wilaya/Halmashauri. Wajumbe wengine wa kamati ni Afisa Ardhi, Afisa Mazingira, Afisa Mipango Miji na Vijiji, Mwanasheria, Afisa mifugo wa Kata na mjumbe yeyote atakaye onekana anahitajika kutokana na umuhimu wake.

c) Kamati ya Usimamizi wa maeneo ya malisho ya ngazi ya Kata

(i) Mwenyekiti wa Kamati hii atakuwa Mtendaji wa Kata na katibu atakuwa Afisa mifugo wa kata. Wajumbe wengine watakuwa kiongozi wa Chama cha Wafugaji ngazi ya kata, maafisa mifugo wa vijiji husika vilivyo ndani ya kata

(ii) Kamati hii itashirikiana na Serikali za Vijiji husika kulinda maeneo ya malisho na kutunza vyanzo vya maji vilivyopo ambavyo vinasaidia katika upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo.

d) Kamati ya Usimamizi wa Maeneo ya Malisho ngazi ya Kijiji

(i) Mwenyekiti wa Kamati hii atakuwa ni yule aliyechaguliwa na ushirika wa wafugaji ulioundwa katika ngazi ya kijiji kwa lengo la kusimamia eneo la malisho la kijiji na katibu atakuwa ni Afisa mifugo anayesimamia kijiji husika. Wajumbe wengine watakuwa ni Mwenyekiti wa timu ya mipango ya

matumizi ya ardhi ya kijiji (VLUM) na mjumbe mmoja kutoka Chama cha Wafugaji ngazi ya kijiji na mtunza hazina wa kamati ya usimamizi wa malisho ngazi ya kijiji (Rejea sura Na. 2.1.3 (c)).

(ii) Kamati hii itashirikiana na Serikali ya kijiji ili kulinda maeneo ya malisho na kutunza vyanzo vya maji vilivyopo ambavyo vinasaidia katika upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo.

e) Kamati ya usimamizi wa maeneo ya malisho ya pamoja

(i) Kamati hii itaundwa na wajumbe wawili kutoka kwenye kamati ya usimamizi wa malisho ngazi ya vijiji vinavyoungana na kutumia malisho ya pamoja.

(ii) Mwenyekiti wa Kamati hii atakuwa ni kiongozi kutoka miongoni mwa viongozi wa Kamati za usimamizi wa malisho za vijiji vilivyoungana,

(iii) Katibu wa Kamati hii atakuwa ni mmoja wa viongozi/mjumbe kutoka chama cha wafugaji ngazi ya kijiji kutoka vijiji vilivyoungana.

(iv) Jukumu la Kamati hii ni kusimamia na kuendeleza maeneo yote ya malisho yaliyoungana kutoka katika vijiji husika.

### 4.3.1 Majukumu ya wadau katika upatikanaji, usimamizi na uendelezaji wa malisho na mbegu za malisho.

Malisho bora hutokana na uwepo wa mbegu bora hivyo basi kutokana na uhaba wa mbegu bora za malisho nchini wadau

wote wanapaswa kuhusika katika uzalishaji wa mbegu za malisho.

#### 4.3.2 Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika upatikanaji wa mbegu za malisho.

a) Kuhamasisha na kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri kuanzisha mashamba ya uzalishaji wa mbegu za malisho na kuwa na mashamba darasa ya kuzalisha mbegu za malisho katika ngazi za vijiji;

b) Kurahisisha na kuweka utaratibu mzuri wa uagizaji wa mbegu za malisho kutoka nje ya nchi kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) na Wizara ya Kilimo;

c) Kuwezesha mashamba ya malisho yaliyopo chini ya Wizara na Taasisi zake kuongeza uzalishaji wa mbegu;

d) Kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza na kushiriki katika uzalishaji wa mbegu za malisho;

e) Kuwezesha uthibitishaji wa mbegu za malisho kwa kushirikiana na Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) na TALIRI kulingana na kanuni za kusimamia mbegu za malisho;.

f) Kutoa elimu ya uzalishaji, uvunaji na uhifadhi wa mbegu za malisho kwa maafisa ugani ngazi zote ambao watatoa elimu hiyo kwa wafugaji ili kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za malisho.

### 4.3.3 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri katika upatikanaji wa mbegu za malisho.

a) Kuhamasisha na kusimamia uanzishwaji wa mashamba kwa ajili ya uzalishaji wa malisho na mbegu kwenye Vijiji;

b) Kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika uzalishaji wa mbegu za malisho;

c) Kutoa elimu ya uzalishaji, uvunaji na uhifadhi wa mbegu za malisho kwa wafugaji ili kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za malisho;

d) Kuwasimamia Wakaguzi wa maeneo ya malisho kukagua mashamba yanayozalisha mbegu yaliyopo ndani ya Wilaya na kutoa taarifa ngazi ya Wizarani katika kila robo ya mwaka;

e) Kusimamia uvunaji wa mbegu na uhifadhi wa mbegu katika mashamba ya mbegu yaliyopo katika vijiji na wilaya kupitia Wakaguzi wa Maeneo ya Malisho;

f) Halmashauri zihamasishe uanzishwaji na usimamizi wa mpango wa kopa mbegu lipa mbegu za malisho ili kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbegu za malisho.

### 4.3.4 Majukumu ya Wafugaji katika upatikanaji wa mbegu za malisho.

a) Kuanzisha na kusimamia mashamba mapya ya malisho katika eneo lililotengwa kwa ajili ya malisho ili kuongeza uzalishaji wa mbegu za malisho;

b) Kuvuna na kuhifadhi mbegu za malisho kwa kuzingatia kanuni na ushauri wa wataalam waliopo eneo husika;

c) Kuongeza uzalishaji wa mbegu za malisho kwa kila mwaka ili kukidhi mahitaji ya mbegu nchini.

# SURA YA TANO

## 5.0 UPATIKANAJI NA USIMAMIZI WA MAJI KWA MIFUGO

### 5.1 Upatikanaji wa Maji.

Maji ni Rasilimali muhimu kwa ajili ya ustawi wa malisho na mifugo, Rasilimali hii kwa mifugo inapatikana kwa njia za asili au kwa kuchimba Visima, Malambo, Mabwawa au Miundombinu yoyote inayohusika na huduma za maji kwa mifugo. Ili kuwezesha upatikanaji wa maji kwa mifugo, wafugaji wanahamasishwa kujiunga kwenye vikundi au ushirika kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kuchangia fedha ili kujenga/kukarabati visima/malambo/mabwawa. Ujenzi/ukarabati huo utafanyika kwa kushauriwa na wataalam wa mifugo kwa kushirikiana na watalaam wa maji.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maji, Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri, wafugaji na wadau wengine watashirikiana ili kuhakikisha ujenzi wa malambo/mabwawa na uchimbaji visima virefu katika maeneo ya malisho unazingatia uwiano uliopo wa mahitaji ya mifugo. Wadau zikiwemo Wizara, Sekta Binafsi na Taasisi mbalimbali zinapotekeleza miradi yake, ziangalie uwezekano wa kuweka/kujenga mifumo ya maji kwa mifugo; mfano, mashimo yanayopatikana wakati wa ujenzi wa barabara. Mashimo hayo yachimbwe kimkakati ili baadaye yatengenezwe kuwa malambo ya maji kwa ajili ya mifugo.

Ni wajibu wa wafugaji kuhakikisha kuwa rasilimali hiyo ya maji inayopatikana inatunzwa, kutumiwa na kuendelezwa kwa kuzingatia kanuni muhimu zifuatazo:-

a. Kuweka utaratibu wa njia zitakazowezesha mifugo kuyafikia maji
b. Kuboresha upatikanaji wa maji na kuhakikisha yanatumika kwa ufanisi na kuhifadhiwa;
c. Wadau na walengwa kushirikishwa katika ngazi zote za usimamizi, matumizi na usalama wa rasilimali za maji kwa mifugo na miundombinu yake;
d. Kuboresha usimamizi na hifadhi ya mifumo ya ikolojia na bayoanuai;
e. Kuzuia na kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa rasilimali za maji kwa mifugo;

## 5.2 Majukumu ya Wadau katika Upatikanaji wa Maji kwa Mifugo.

### 5.2.1 Majukumu ya Wafugaji

a) Kuhakikisha wanashiriki katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo;
b) Kutumia teknolojia rahisi (appropriate technology) za uvunaji na uhifadhi wa maji kwa ajili ya mifugo;
c) Kutunza mazingira na kusimamia utumiaji wa miundombinu ya maji katika ufugaji (mabwawa/malambo, visima virefu na mabirika/mbauti);
d) Kusimamia na kulinda njia za mifugo kuelekea kwenye mabirika/mbauti na malisho ili kuepuka uvamizi;
e) Kuweka utaratibu wa kupata fedha au kuchangia gharama ya uendeshaji na ukarabati wa miundombinu ya maji ili iwe endelevu.

### 5.2.2 Majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri

a) Kutenga na kutumia asilimia 15 ya mapato yatokanayo na mifugo (Waraka wa Rais Na. 1 wa Mwaka 2002) kwa ajili ya kujenga na kukarabati miundombinu ya maji na huduma nyingine za mifugo;

b) Kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika kujenga miundombinu ya maji;

c) Kuhamasisha uwekezaji katika matumizi ya teknolojia ya uvunaji na usambazaji wa maji kwa ajili ya malisho na mifugo;

d) Kuhamasisha wadau wa sekta binafsi na wafugaji kuhakikisha wanajenga na kukarabati malambo/mabwawa na kuchimba visima virefu katika maeneo ya malisho kwa uwiano unaozingatia mahitaji ya Mifugo;

e) Kusimamia miundombinu ya maji ya mifugo katika Halmashauri.

### 5.2.3 Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi

a) Kujenga na kukarabati miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo;

b) Kuhamasisha Wizara ya Maji, Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri na wadau wengine kuhakikisha wanajenga, wanakarabati na kusimamia matumizi ya malambo/mabwawa na kuchimba visima virefu katika maeneo ya malisho kwa uwiano unaozingatia mahitaji ya Mifugo;

c) Kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika kujenga na kukarabati miundombinu ya maji kwa mifugo;

d) Kuhamasisha wafugaji kujenga, kukarabati na kusimamia matumizi ya miundombinu ya maji kwa mifugo;

e) Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Halmashauri kufuatilia Wizara ya Ujenzi ili mashimo yanayobaki wakati wa ujenzi wa barabara yachimbwe kimkakati kwa lengo la kuyatengeneza kuwa malambo ya maji kwa ajili ya mifugo;

f) Kuhamasisha uwekezaji katika matumizi ya tekinolojia ya uvunaji na usambazaji wa maji kwa ajili ya malisho na mifugo.

### 5.2.4 Majukumu ya Wizara ya Maji

Kusimamia Sera na Sheria za Maji ili kuwezesha upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo.

## 5.3 Usimamizi wa Miundombinu ya Maji kwa ajili ya Mifugo

Kamati iliyoundwa kwa lengo la kusimamia maeneo ya malisho, itahusika kusimamia miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo kwa kuzingatia majukumu yaliyoanishwa kwenye mwongozo huu. pamoja na majukumu hayo katika kusimamia miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo Kamati itazingatia vifungu Na. 32 na 33 vya Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 12 ya Mwaka 2009 na marekebisho yake.

### 5.3.1 Majukumu ya Kamati katika kusimamia na kuhifadhi miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo

a) Kulinda miundombinu ya maji;

b) Kuweka utaratibu wa kuchangisha fedha kutoka kwa watumia maji ili zitumike kukarabati miundombinu ya maji inapoharibika;

c) Kutoa elimu ya matumizi bora ya huduma za maji kwa ajili ya shughuli za mifugo;

d) Kuzuia watu na mifugo kupata maji moja kwa moja kutoka kwenye mabwawa/malambo au visima isipokuwa kwenye maeneo maalumu (mabirika/mbauti) yaliyoainishwa kwa ajili ya kazi hiyo;

e) Kusafisha mabirika/mbauti mara kwa mara;

f) Kuweka makatazo ya kuoga, kuoshea vitu na kuogelea kwenye lambo/bwawa;

g) Kuzungushia uzio kwenye lambo/bwawa/kisima na eneo la kuvunia maji ili kuzuia mifugo kunywa maji moja kwa moja kwenye lambo/bwawa/kisima, kwa lengo la kuzuia uharibifu;

h) Kuotesha majani katika njia ya kuingia maji kwa lengo la kuzuia mmomonyoko na kuchuja maji yasiingize tope kwenye lambo/bwawa kwa kuzingatia ushauri wa kitaalam;



***Picha Na.7: Madhara ya kunywesha mifugo ndani ya bwawa/lambo***

i) Kamati ya kusimamia maeneo ya malisho na maji ina wajibu wa kuhakikisha kuwa mbauti/birika inafanya kazi muda wote kwa kuweka utaratibu wa kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kufanya ukarabati kwa uharibifu utakaojitokeza wakati wa kutumia bwawa/lambo/kisima na birika/mbauti,
ii. Kusafisha birika/mbauti mara kwa mara,
iii. Kusafisha mabomba ya kuingiza na kutoa maji ili kuhakikisha kuwa maji yanapatikana muda wote,
iv. Kufuatilia bomba la kutoka kwenye bwawa/lambo/kisima ili kuhakikisha kuwa halivuji na hivyo kuzuia upotevu wa maji,



***Picha Na. 8. Mifugo inayokunywa maji kwenye birika/mbauti na sio moja kwa moja kwenye bwawa/lambo/kisima***

# SURA YA SITA

## 6.0 SHERIA ZITAKAZOTUMIKA PAMOJA NA MWONGOZO HUU

Katika Mwongozo huu, Sheria na Kanuni mbalimbali zitatumika. Miongoni mwa Sheria hizo ni pamoja na:-

a) Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura Na 180. (Sheria hii pamoja na mambo mengine inampa mamlaka Mkurugenzi kusajili maeneo ya malisho na kuyapendekeza ili yatangazwe kwenye Gazeti la Serikali).

b) Sheria ya Ushirika Sura Na. 337. (Ushirika ni dhana ya kuleta maendeleo kwa kushirikiana na kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Kufuatana na Sheria hii watu kuanzia 20 wanaweza kuunda Ushirika).

c) Sheria ya Usajili wa Vyama (Inasajili vyama mbalimbali vya wafugaji).

d) Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Sura Na.116. (Sheria hii inaelekeza taratibu za upatikanaji wa maeneo ya malisho kupitia uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi).

e) Sheria ya Ardhi ya vijiji Sura Na.114 na Kanuni zake, Kanuni za Mwaka 2002 kifungu cha 25 – 35. (Kwa mujibu wa kifungu 25 mwenye mamlaka ya kugawa na kutoa hati ya umiliki wa ardhi kimila ni Halmashauri ya Kijiji).

f) Sheria ya Serikali za Mitaa Sura Na.288. (Sheria hii inaonyesha Mamlaka ya viongozi waliopo katika ngazi ya Wilaya ambao wana majuhumu muhimu ya kutafuta/kubainisha, kusimamia na kulinda maeneo ya malisho).

g) Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo Sura Na.120.(Sheria hii inasaidia kuyalinda maeneo ya malisho na kutoa fursa ya ufugaji endelevu kwa kuzingatia uwiano baina ya ukubwa wa eneo na idadi ya mifugo. Vile vile inasaidia kudhibiti uhamaji holela wa mifugo na utambuzi wa haraka wa mifugo inakotoka).

h) Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Sura Na.216.(Sheria hii inasaidia kupunguza/kuondoa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006)

i) Sheria ya Ustawi wa Wanyama Sura Na. 154 (Sheria hii inatoa haki ya mifugo kupata huduma muhimu kama vile maji na malisho. Hivyo, inahamasisha maeneo yote ya malisho kuwa na maji na malisho bora kwa ajili ya mifugo)

j) Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Sura Na. 156. (Sheria hii inasaidia kuzuia uambukizaji wa magonjwa ya mifugo toka eneo moja kwenda lingine ambapo huathiri upatikanaji na uboreshaji wa maeneo ya malisho).

k) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira sura Na.191 (Sheria hii inasaidia kuwepo na ufugaji endelevu usioharibu mazingira).

l) Sheria ya Misitu sura Na. 323. (Sheria hii inalinda vyanzo vya maji ambavyo vingi hupatikana katika hifadhi nzuri za misitu).

m) Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Sura Na.272 (Sheria hii inaongeza usimamizi na uhifadhi maji na vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kulinda miundombinu ya maji na kuzuia mifugo na wanyama pori kunywa maji moja kwa moja kwenye lambo/bwawa).

n) Sheria ya Hifadhi ya Wanyama pori sura Na.283.

o) Sheria ya Ardhi Na.4 ya Mwaka 1999

p) Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya Mwaka 1999.

**6.1 Maadili ya Kuzingatia katika Utekelezaji wa Mwongozo**

Katika kutekeleza mwongozo huu wadau wote watatakiwa kuzingatia maadili yafuatayo:-

a) Kutenda haki kwa wadau wote,

b) Kutopokea au kutoa rushwa,

c) Kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu zote,

d) Kutoa ushirikiano kwa wadau wote,

e) Kufanya kazi kwa uadilifu na weledi.

# SURA YA SABA

## 7.0 MATOKEO TARAJIWA YA MWONGOZO

Maeneo ya malisho yamekuwa yakipungua na kupoteza ubora wake kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ongezeko la idadi ya watu, Maeneo ya Hifadhi, makazi, kilimo na shughuli nyingine za kijamii na kiuchumi. Wakati nchi inapata uhuru idadi ya watu ilikuwa milioni 9 na kwa sasa idadi ya watu inakadiriwa kufikia takriban milioni 60 mwaka 2019/2020.

**Mwongozo unatarajiwa kuwa na matokeo yafuatayo:-**

(i) **Upatikanaji wa uhakika wa malisho na maji kwa mifugo.**
Mwongozo huu utawawezesha wafugaji kuwa na uhakika wa umiliki wa maeneo ya malisho ambayo watayaendeleza na hivyo kuwa na uhakika wa upatikanaji wa malisho na maji kwa kipindi chote cha mwaka.

(ii) **Kupungua kwa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.**
Mwongozo huu utawezesha maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho kuwekewa ulinzi wa kutosha ambapo wafugaji wenyewe watakuwa na wajibu wa kulinda maeneo au vitalu watakavyokabidhiwa na hivyo kupunguza migogoro inayojitokeza ya kundi moja kuvamia maeneo yanayotumiwa na wengine.

(iii) **Ufugaji wa kisasa na wenye tija.**

Mwongozo huu unatoa fursa kwa wafugaji kukusanyika pamoja na kupewa elimu ya ufugaji bora na wenye tija. Elimu hiyo ni pamoja na uzalishaji, uendelezaji na uhifadhi wa malisho, unenepeshaji wa mifugo, uhimilishaji, matumizi ya madume bora, ufugaji unaozingatia uwiano wa eneo na idadi ya mifugo na uvunaji wa mifugo. Wafugaji wataelimishwa kuhusu umuhimu wa kuendeleza miundombinu ya mifugo na malisho

(iv) **Ongezeko la uzalishaji wa mbegu za malisho**.

Mwongozo unaelekeza kuhusu namna ya kuongeza upatikanaji na matumizi ya mbegu bora za malisho.

(v) **Uundaji wa Ushirika na Vikundi vya Wafugaji**

Mwongozo huu unatoa fursa kwa wafugaji kupewa elimu ya Ushirika na uundaji wa vyama ama vikundi ili wajiunge pamoja katika Ushirika na vikundi vyao wao kwa hiari na kufanikisha azma yao ya kupata mahitaji ya kijamii na kiuchumi ikiwemo upatikanaji wa mikopo.

(vi) **Kuwepo kwa utii wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusu usimamizi na uendelezaji wa maeneo ya malisho**

Mwongozo huu unaelekeza wafugaji na wadau wengine kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu katika usimamizi na uendelezaji maeneo ya malisho.



***Picha Na. 9. Ng'ombe wakiwa kwenye malisho yaliyoboreshwa***

**Kiambatisho Na 1: Mchanganuo wa maeneo ya malisho katika Halmashauri**

Mkoa wa .................................... Halmashauri ya ..................................

| Na. | Jina la eneo la malisho | Kijiji | Ukubwa (ha) | Majira nukta (Coordinates) ya eneo la malisho | | Idadi ya vitalu kulingana na ukubwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Eastings | Northings | |
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | | | | | | |
| 5. | | | | | | |
| 6. | | | | | | |
| 7. | | | | | | |
| 8. | | | | | | |
| 9. | | | | | | |
| 10. | | | | | | |
| 11. | | | | | | |
| 12. | | | | | | |
| 13. | | | | | | |
| | Jumla | | | | | |

## Kiambatisho Na. 2: Mchanganuo wa maeneo ya malisho kwa Taasisi

Mkoa wa ........................................ Wilaya ya ........................................

| Na. | Jina la eneo la malisho | Kijiji | Ukubwa (ha) | Majira nukta (Coordinates) ya eneo la malisho | | Idadi ya vitalu kulingana na ukubwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Eastings | Northings | |
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | | | | | | |
| 5. | | | | | | |
| 6. | | | | | | |
| 7. | | | | | | |
| 8. | | | | | | |
| 9. | | | | | | |
| 10. | | | | | | |
| 11. | | | | | | |
| 12. | | | | | | |
| 13. | | | | | | |
| | **Jumla** | | | | | |

**Kiambatisho Na. 3: Kanda kuu za kiikolojia na aina ya malisho yanayofaa kupandwa**

| Kanda za hali ya hewa (Climatic zones) | Maelezo | Mifano ya maeneo | Aina ya malisho stahili |
|---|---|---|---|
| 1) Maeneo ya miinuko yenye unyevunyevu (Wet Montane) | Safu za milima kati ya mita (m) 1,200 juu ya usawa wa bahari na mwanzo wa ukanda wa theluji, ambapo kuna mvua nyingi isiyopungua milimita (mm) 1,000 kwamwak a. Kiwango cha chini cha joto ni 130C. Kuna ukungu na mawingu mara kwa mara | Lushoto, Magamba, Narok, Bunduki, Mufindi, Tukuyu, Ngorongoro | 1. Majani<br>*Lolium perenne*<br>*Chloris gayana*<br>*Pennisetum purpureum*<br>*Setaria splendida*<br>*Tripsacum fasciculatum*<br><br>2. *Mikunde kunde*<br>*Trifolium spp*<br>*Desmodium intortum*<br>*Neonotonia wightii*<br>*Lablab purpureum*<br>*Medicago sativa*<br><br>3. *Miti Malisho*<br>Calliandra calothyrsus<br>Leucaena diversifolia<br>Acacia angustissima |
| 2) Maeneo ya miinuko yenye | Maeneo ya milimani kati ya m | Shume, Njombe, | 1. Majani<br>*Setaria splendida* |

| Kanda za hali ya hewa (Climatic zones) | Maelezo | Mifano ya maeneo | Aina ya malisho stahili |
|---|---|---|---|
| ukame (Dry montane) | 1,200 juu ya usawa wa bahari na mwanzo wa ukanda wa theluji, ambapo kwa kawaida mvua ni chini ya mm 760 kwa mwaka. Kiwango cha chini cha joto ni $13^0C$ | Iringa, Meru Kaskazini, Hanang | *Setaria anceps*<br>*Panicum maximum*<br>*Chloris gayana*<br>*Pennisetum purpureum*<br>*Brachiaria spp*<br>*Tripsacum fasciculatum*<br>*Cenchrus ciliaris*<br><br>2. *Mikunde kunde*<br>*Neonotonia wightii*<br>*Desmodium uncinatum*<br>*Desmodium intortum*<br>*Centrosema pubescens*<br>*Pueraria phaseoloides*<br>*Colopogonium mucunoides*<br>*Macroptilium atropurpureum*<br>*Medicago sativa*<br><br>3. *Miti Malisho*<br>Leucaena |

| Kanda za hali ya hewa (Climatic zones) | Maelezo | Mifano ya maeneo | Aina ya malisho stahili |
|---|---|---|---|
| | | | leucocephala<br>Calliandra calothyrsus<br>Grilicidia sepium<br>Acacia angustissima |
| 3) Maeneo ya miinuko ya wastani (Transitional montane) | Maeneo ya milimani kati ya m 1,200 juu ya usawa wa bahari na Mwanzo wa ukanda wa theluji yenye hali ya hewa kati ya (1) na (2) | Sungwi, Olmotonyi, Rongai, Mbulu, Mbeya | 1. Majani<br>Setaria splendida<br>Setaria anceps<br>Panicum maximum<br>Chloris gayana<br>Pennisetum purpureum<br>Brachiaria spp<br>Tripsacum fasciculatum<br>Cenchrus ciliaris<br><br>2 Mikunde kunde<br>Trifolium spp<br>Neonotonia wightii<br>Desmodium uncinatum<br>Desmodium intortum<br>Centrosema pubescens<br>Pueraria phaseoloides |

| Kanda za hali ya hewa (Climatic zones) | Maelezo | Mifano ya maeneo | Aina ya malisho stahili |
| --- | --- | --- | --- |
| | | | Colopogonium mucunoides<br>Macroptilium atropurpureum<br>Medicago sativa<br>Lablab purpureum<br><br>3. Miti Malisho<br>Leucaena leucocephala<br>Calliandra calothyrsus<br>Grilicidia sepium<br>Acacia angustissima |
| **4) Nyanda za juu zenye unyevunyevu (Moist plateau)** | Maeneo kati ya m 600 na m 1,200 juu ya usawa wa bahari yenye mvua kati ya mm 760 na 1,140 kwa mwaka. Kiwango cha chini cha joto ni $13^0C$ | Geita, Mpanda, Tabora, Kigoma, Moshi | 1. Majani<br>Chloris gayana,<br>Setaria anceps,<br>Panicum maximum,<br>Panicum coloratum<br>Panicum antidotale<br>Cenchrus ciliaris<br>Guatemala<br><br>2. Mikunde kunde<br>Medicago sativa<br>Neonotonia |

| Kanda za hali ya hewa (Climatic zones) | Maelezo | Mifano ya maeneo | Aina ya malisho stahili |
|---|---|---|---|
| | | | wightii<br>Clitoria ternatea<br>Stylosanthes spp<br>Macroptiluim atropurpureum<br>Centrosema pubescens<br>3. Miti Malisho<br>Leucaena leucocephala<br>Grilicidia sepium<br>Cajanus cajan<br>Morus alba<br>Leucaena pallida,<br>Leucaena diversifolia |
| 5) Nyanda za juu zenye ukame (Dry plateau) | Maeneo kati ya m 600 na m 1,200 yeye mvua chini ya mm 760 kwa mwaka. Kiwango cha chini cha joto ni $13^0C$ | Dodoma, Itigi, Mwanza, Shinyanga, Tabora. | 1. Majani<br>Cenchrus ciliaris<br>Cynodon spp<br>Chloris gayana<br>Bothriochloa spp<br>Panicum coloratum<br><br>2. Mikunde kunde<br>Stylosanthes spp<br>Centrosema pubescens<br>Clitoria ternatea<br>Macroptiluim atropurpureum |

| Kanda za hali ya hewa (Climatic zones) | Maelezo | Mifano ya maeneo | Aina ya malisho stahili |
|---|---|---|---|
| | | | Lablab purpureus<br><br>3. Miti Malisho<br>Leucaena leucocephala<br>Sesbania sesban<br>Grilicidia sepium<br>Cajanus cajan<br>Leucaena pallida,<br>Leucaena diversifolia |
| 6) Maeneo ya hali ya joto na unyevunyevu (Wet tropical) | **Maeneo maalum katika mwambao wa pwani, chini ya milima yenye mvua nyingi, na maeneo ya tambarare yaliyoko mashariki mwa baadhi ya milima. Mvua mm 1,140 au zaidi kwa mwaka. Kiwango cha chini cha joto ni 13$^0$C** | Rau,<br>Matombo,<br>Minziro,<br>Ukerewe,<br>Korogwe,<br>Muheza,<br>Gonja<br>Maore,<br>Kyela,<br>Turiani,<br>Bukoba | 1. Majani<br>Chloris gayana,<br>Setaria anceps,<br>Panicum maximum,<br>Panicum coloratum<br>Panicum antidotale<br>Cenchrus ciliaris<br>Guatemala<br><br>2. Mikunde kunde<br>Medicago sativa<br>Neonotonia wightii<br>Clitoria ternatea<br>Stylosanthes spp<br>Macroptiluim atropurpureum |

| Kanda za hali ya hewa (Climatic zones) | Maelezo | Mifano ya maeneo | Aina ya malisho stahili |
|---|---|---|---|
| | | | Centrosema pubescens<br><br>3. Miti Malisho<br>Leucaena leucocephala<br>Grilicidia sepium<br>Cajanus cajan<br>Morus alba<br>Leucaena pallida,<br>Leucaena diversifolia |
| 7) Mwambao wa pwani (Coastal belt) | **Ukanda wa pwani chini ya m 600 juu ya usawa wa bahari. Sehemu zingine huingia bara hadi kilomita (km) 300 Kwa mfano Ifakara). Mvua kwa kawaida ni mm 1,000 kwa mwaka. Kiwango cha chini cha joto ni 18$^0$C** | Dar-es-Salaam Kibaha, Bagamoyo, Lindi, Ifakara. Mtwara, Rufiji | 1. Majani<br>*Setaria splendida*<br>*Setaria anceps*<br>*Panicum maximum*<br>*Chloris gayana*<br>*Pennisetum purpureum*<br>*Brachiaria spp*<br>*Tripsacum fasciculatum*<br>*Cenchrus ciliaris*<br><br>2. *Mikunde kunde*<br>*Neonotonia wightii*<br>*Desmodium uncinatum*<br>*Desmodium* |

| Kanda za hali ya hewa (Climatic zones) | Maelezo | Mifano ya maeneo | Aina ya malisho stahili |
|---|---|---|---|
| | | | *intortum*<br>*Centrosema pubescens*<br>*Pueraria phaseoloides*<br>*Colopogonium mucunoides*<br>*Macroptilium atropurpureum*<br>*Medicago sativa*<br><br>3. *Miti Malisho*<br>Leucaena leucocephala<br>Calliandra calothyrsus<br>Grilicidia sepium<br>Acacia angustissima |